

HABARI KUHUSU VELENJE

Velenje ni mji mchanga na wa kisasa barani Ulaya ulio na majengo ya kisasa na uwazi unaoongezeka wa mwingiliano wa tamaduni. Katika karne ya 13, ulitajwa kwanza kama mji wa soko, ukaanza kukua kama mji baada ya Vita vya Pili vya Ulimwengu; mnamo tarehe 20 Septemba 1959, katikati mwa mji huo uliotoka kujengwa ulifunguliwa rasmi. Leo, Velenje pia ni manispaa ya mji, inayojumuisha vijiji 25 vya watu karibu 33,000, ambapo karibu 25,000 wanaishi mjini humo. Ni moja ya vituo muhimu vya kiuchumi vya Slovenia pamoja na kituo cha ajira, utawala na elimu katika Mkoa wa Savinja-Šalek. Nguzo za maendeleo ya kiuchumi ya Velenje ni pamoja na madini ya makaa ya mawe, sekta ya nishati, uhunzi na huduma maalumu; hivi karibuni pia utalii. Miundombinu na ukarimu wa Velenje uliohifadhiwa vyema ulipokea tuzo nyingi kwa kiwango cha kitaifa na kimataifa. Hali asili katika mji huo (kimo cha mita 390 – Uwanja wa Tito) na mazingira yake inaonekana na kuweza kufikika kwa urahisi: katika mbuga za mji, misitu, na maziwa, kwenye vijia vya matembezi, vya baiskeli na vya milima. Vifaa vya kisasa vya michezo, taasisi za kitamaduni, makumbusho, taasisi za elimu na jamii, vilabu na watu wengi wenye ubunifu wanachangia pakubwa katika umaarufu wa mji huo. Velenje unajulikana kwa matukio yake mengi ya michezo, burudani, utalii na tamaduni. Ni mji wa muziki, ngoma, mashairi, na mawazo yanayochipuka. Majina mengi maarufu yataandika historia ya Velenje: wanauchumi, wanasayansi, wasanii, wanariadha, wanasiasa n.k. wanaotambulika wanatoka Velenje. Velenje ni mji ulio na minara ya ukumbusho ya kitamaduni, wenye mandhari mengi ya kiasili, na hasa matukio na watu ambao wanakualika na kukutazamia kwa hamu sana. – *Karibuni Velenje, marafiki wa zamani na wapya!*